



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

Yah: UHUISHAJI WA LESENI ZA UUGUZI NA UKUNGA KWA MSIMU  
WA MWAKA 2023-2026

**Dodoma, 11 Julai, 2023.**

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania ni mamlaka ya Kisheria iliyoanzishwa kwa ajili ya kusimamia Wataaluma na Taaluma za Uuguzi na Ukunga ili kuulinda umma dhidi ya huduma zinazotolewa na Wauguzi na Wakunga nchini. Baraza linafanya kazi chini ya Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010 na Kanuni zake.

Uhuishaji wa Leseni za Uuguzi na Ukunga ni suala la kisheria kama lilivyoelekezwa katika **kifungu cha 21 na 38(1)** cha Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010.

Ofisi ya Msajili inapenda kuwataarifu Wauguzi na Wakunga ambao muda wa matumizi wa Leseni zao unaisha tarehe 31 Disemba, 2023 kwamba dirisha la kuhuisha leseni limefunguliwa tangu tarehe 01/07/2023 kwa gharama za kawaida bila faini. Ifikapo tarehe 01/01/2024 gharama hizi zitaambatana na faini.

Kwa tangazo hili, mnaelekezwa kutembelea tovuti ya Baraza <https://tnmcis.tnmc.go.tz/register> ili kukamilisha taratibu za kuhuisha leseni zenu. Aidha, Mwongozo wa namna ya kujisajili na kuhuisha leseni unapatikana katika tovuti hii.

Nawatakia utekelezaji mwema.

Imetolewa na:

  
Agnes Mtawa

**MSAJILI**